

UTT AMIS KWA



MTU

MWENYE HARAKA

MWONGOZO MWEPEZI WA KUWEKEZA UTT AMIS



MAOMBI ABEL CHAGAMBA

TEL:0713999596

YALIYOMO


ANGALIZO.....	7
UTANGULIZI	8
SEHEMU YA KWANZA	16
UWEKEZAJI WA PAMOJA NI NINI?	16
UTTT AMIS NI NINI?	18
KIPANDE NI NINI?	21
JINSI FAIDA INVYOKUFIKIA KAMA UMEWEKEZA UTT AMIS	22
1) KUPITIA GAWIO	22
2) KUPITIA UKUAJI WA MTAJI	23
FAIDA ZA KUWEKEZA UTT AMIS	24
MREJESHO WA UWEKEZAJI	28
SHEHEMU YA PILI	29
MFUKO WA UMOJA.....	31
MFUKO WA WEKEZA MAISHA	35
MFUKO WA WATOTO.....	43
MFUKO WA JIKIMU	47
MFUKO WA UKWASI	51
MFUKO WA HATI FUNGANI.....	54
SEHEMU YA TATU	58
JINSI YA KUANZA KUWEKEZA KWA MARA YA KWANZA	58
JINSI YA KUKAMILISHA USAJILI	60
JINSI YA KUUZA VIPANDE VYAKO.....	60
JUA GHARAMA AMBAZO UNAINGIA WAKATI WA KUWEKEZA	61
JINSI YA KUTOA FAIDA NA KUBAKIZA MTAJI	62
MIFUKO YENYE HISA NA MIFUKO ISIYO NA HISA	64
JE MFUKO UNATOA GAWIO NI BORA KULIKO USITOA GAWIO?	65
JINSI YA KUJUA BEI YA KIPANDE.....	65
UWEKEZAJI WA MARA MOJA NA UWEKEZAJI WA MARA KWA MARA.....	66
MPANGO WA KUWEKEZEWA GAWIO (RE-INVESTMENT) MPANGO BORA WA UTT AMIS.	68
JINSI YA KUTENGENEZA PENSHENI YAKO.	70


UTT AMIS VS NYUMBA 72

MAWASILIANO NA KAMPUNI YA UTT AMIS. 76

REFERENCES 77

VITABU VINGINE VYA MWANDISHI





Vitabu hivi viko katika mfumo wa E BOOK. (bei ya kila kitabu ni 5000/=)

Lipa 5000/= kwa TIGOPESA 0713999596 (MAOMBI CHAGAMBA) kisha tuma sms ya malipo kwenda WHATSAPP NO 0713999596 ukiambatanisha jina la kitabu na utapokea kitabu ndani ya masaa 12

©Maombi A. Chagamba

Simu: +255713999596,

WhatsApp: +255713999596 au

Email wiseinvestorr@gmail.com

JINSI YA KUSOMA KITABU HIKI

Kitabu hiki kimegawanyika katika sehemu kuu 4, sehemu ya kwanza ni utangulizi na hapa nimezungumzia namna ya kuanza kuwekeza na kutoa picha ya jumla ya uwekezaji katika mfuko wa UTT AMIS, sehemu ya pili ni muongozo wa mifuko ya UTT AMIS, na sehemu ya tatu ni namna ya kusimamia uwekezaji wako ikiwa ni pamoja na jinsi ya kuwekeza kwa faida kubwa katika mfuko huu.

ANGALIZO

Kitabu hiki kimetolewa kwa lengo la kutoa uelewa wa masuala ya uwekezaji katika mfuko wa uwekezaji wa pamoja wa UTT AMIS. Mwandishi ameandika haya aliyoyawasilisha kwenye kitabu hiki kutokana na uelewa wake juu ya masuala ya uwekezaji katika mfuko wa Pamoja wa UTT AMIS na uwekezaji katika masoko ya mitaji. Uelewa na elimu aliyoiwasilisha katika kitabu hiki imetokana na kujifunza kupitia kusoma, semina na kuwekeza kwenye mifuko mbalimbali iliyo chini ya UTT AMIS lakini pia kwenye vyanzo vingine vya mapato vilivyo kwenye soko la hisa la Dar Es Salaam.

Mwandishi sio mshauri wa masuala ya fedha au uwekezaji isipokuwa ni mwekezaji na mtu aliye na ufahamu kuhusu masuala ya uwekezaji, kama msomaji atahitaji kuwekeza sehemu yoyote iliyoelezwa kwenye kitabu hiki, anashauriwa awaone wataalamu wa masuala ya fedha na uwekezaji kwa ajili ya kupata ushauri mahsusi kabla ya kuwekeza.

Mwandishi hatahusika na kitendo chochote ambacho kitachukuliwa na msomaji kutokana na taarifa zilizopo katika kitabu hiki, ieleweke kuwa kilichoandikwa humu ni maoni ya mwandishi na wala hayahusiani na UTT AMIS wala chombo chochote kilichotajwa katika kitabu hiki. Pia mwandishi sio mfanyakazi wa UTT AMIS na wala hana mahusiano yoyote na mifuko hii. Kwa maelezo zaidi kuhusu UTT AMIS unaweza kuwasiliana na mfuko wa UTT AMIS kupitia mawasiliano yaliyo mwisho wa kitabu.

UTANGULIZI

Kama haujawahi kuwekeza kabisa, ngoja nikupe hatua ambazo kila mtu anapitia ili kufikia uhuru wa kifedha (financial freedom)

- 1) Kupata pesa
- 2) Kuzalisha pesa
- 3) Kutunza pesa (protect money)

Kila mtu hapa duniani anapata pesa kwa namna moja au nyingine katika vipindi tofauti vya maisha yake ila changamoto inakuja katika vipengele viwili vya kuzalisha pesa na kutunza (protect) pesa, asikudanganye mtu ya kuwa unaweza kufikia uhuru wa kifedha kwa kupata pesa tu, wengi wetu tuna ujuzi ambao tumeupata kutoka shuleni ambao unatuwezesha kupata pesa, tumetumia miaka mingi kupata ujuzi huu na hatimaye tukapata kazi.

Kupata kazi ambayo inaingiza mshahara ni hatua moja bora na ya msingi sana ya kuelekea uhuru wa kifedha ila ni hatua ya kwanza kabisa bado kuna hatua mbili ambazo unatakiwa kuzichukua

MFANO WA MKULIMA.

Wengi wetu tunategemea chakula ambacho kinazalishwa na wakulima ili kuishi, ila mkulima huwa anapitia hatua zote tatu ambazo nimezitaja hapo juu, unaweza kuwa na mbegu nyumbani kwako (nafaka) ila hii mbegu kama hauizalishi basi haiwezi kukua, kitendo cha kuwa na mbegu na ukaitumia kinakufanya uwe mtegemezi kila siku wa yule mtu ambaye anatoa mbegu ila ukitaka uhuru lazima ujifunze kuzalisha mbegu iliyo mkononi mwako.

Pesa ni kama mbegu unaweza kuwa unaipokea kila siku au kila mwezi kupitia mshahara ila kama kila pesa ikija unaitumia tu bila kuizalisha itakubidi kumtegemea yule anayekupa pesa kila mwezi na huu sio uhuru wa kifedha ukitaka uhuru wa kifedha lazima ujifunze kuwa mkulima wa pesa na hapa nina maana unatakiwa kujifunza kuzalisha pesa

MFANO WA 2

Miaka kadhaa iliyopita nilikuwa na changamoto sana ya kifedha ijapokuwa pesa nilikuwa napata nikajiuliza kwa nini siku zote niwe na changamoto ya pesa na jibu nililopata ni kuwa najua kupata pesa ila sijajua jinsi ya kuzalisha pesa kwani pesa inaongezeka pale tu ambapo unajua kuizalisha.

Jaribu kufikiria mfano leo hii una million 1 ni kiviipi unaweza kuibadilisha hii milioni 1 kuwa milioni 10? Hapa utahitaji ujuzi wa kuzalisha pesa, na kiviipi nikikwambia katika kurasa chache zijazo utakuwa umejifuza kuzalisha pesa?

Kama unataka kutoka katika hatua ya kwanza ya kupata pesa basi nikukaribishe katika ulimwengu wa uwekezaji na ninakuahidi ya kuwa baada ya kusoma kitabu hiki utakuwa tayari na uwezo wa kuzalisha pesa.

KOZI FUPI YA UWEKEZAJI.

Ukitaka kuzalisha pesa kama alivyo mkulima itakubidi kujifunza namna ya kulima na kupanda mbegu au unaweza kuwa na pesa ukamwajiri mtu kwa ajili kulima kwa ajili yako,

Sasa katika uzalishaji wa pesa kuna aina mbili za kuzalisha pesa

- 1) Kuzalisha mwenyewe pesa
- 2) Kumpa mtu mwenye ujuzi akuzalishie

Sasa njia ya kwanza inaweza kukuchukua muda mrefu sana mpaka kuwa na ujuzi wa kuwekeza kwa faida mfano ukitaka kuwekeza katika soko la hisa lazima itakubidi kujifunza mengi kama namna soko la hisa linavyofanya kazi na jinsi ya kuchagua kampuni, ila kuna njia ya pili ambayo ndio tutakayoizungumzia hapa kwamba kuna kampuni ambayo iko chini ya umiliki wa serikali chini ya wizara ya fedha ambayo kazi yake kubwa ni kuwekeza kwa ajili yako, hilo halitoshi kampuni hii iko chini ya uangalizi wa benki ya CRDB na imekuwa ikifanya kazi kwa miaka 17 ikiwekeza pesa kwa niaba ya wawekezaji, unachohitaji ni kuwa na pesa na hapa unaweza kuanza kuwekeza hata kama una 5000/= na ukaanza kupata faida za uwekezaji.

Unaweza kuuliza vipi siwezi kupoteza pesa yangu huku? Jibu ni hapana kwani kampuni hii ina wekeza katika maeneo salama na kama bado una wasi wasi ni kuwa mpaka sasa hivi kampuni hii ina wekeza pesa zaidi ya BILIONI 600, nikutoe shaka kuwa kampuni hii ni salama, na mpaka mwisho wa kitabu utakuwa umejifunza mengi kuhusu uendeshaji wa hii kampuni na usalama wake.

Kama utahitaji pesa yako kwa wakati wowote basi utaipata ndani ya siku kumi za kazi au siku tatu za kazi kwa baadhi ya mifuko.

ANGALIZO

Kama unataka utajiri wa haraka basi kitabu hiki hakiwezi kukufaa kabisa

KUWEKA AKIBA VS KUWEKEZA

Kuna utamaduni ambao tunafundishwa wa kuweka akiba, ila kuweka akiba sio kuzalisha pesa, unapopata mbegu ukaihifadhi kwa ajili ya matumizi ya baadae wewe una hekima kuliko mtu ambaye haweke akiba kwani kipindi kijacho wewe utakuwa na mbegu na yeye atakuwa hana, ila akitokea mtu ambaye anazalisha mbegu zake anakuwa bora kuliko wewe uliyeweka akiba.

Ukiwa na laki moja ukaiweka ndani mwaka mzima wewe una nidhamu ya fedha na unastahili pongezi ila kama mwenzako akichukua pesa akaiwekeza kwa mrejesho wa 12% kwa mwaka ina maana mwisho wa mwaka yeye atakuwa na 112000/= wakati wewe uliyeweka akiba utakuwa na 100000/=.

Kama ulikuwa na milioni 10 mwaka 2005 wakati UTT AMIS inaanza kuwekeza pesa kwa niaba ya wawekezaji na ukaiweka akiba basi leo hii utakuwa na 10 milioni ile ile, ila kama ulipata nafasi ya kuwekeza katika mfuko wa UMOJA basi leo hii ungekuwa na zaidi ya milion 120, (milioni mia moja na ishrini) nadhani umeona tofauti kati ya kuweka akiba na kuwekeza.

NIKIWEKA HELA BENKI JE?

Kuna mtu akasema nikiweka hela benki si ni bora kuliko kuwekeza huko UTT AMIS kwani huku benki nitapokea riba, nikamwambia riba unayopokea benki kwa akaunti ya kawaida ni kati ya 2% mpaka 3% kwa mwaka (hapa ina maana kama umewekeza 100000/= basi utapokea 3000/= kama riba) ila huku UTT AMIS unaweza kupata riba ya 12% mpaka 20% kwa baadhi ya mifuko na kwa baadhi ya miaka (ijapokuwa riba hii huwa inabadilika kutegemea na hali ya

uchumi), na hali ya usalama wa pesa yako huku UTT AMIS haina utofauti sana na benki.

SEHEMU SAHIHI YA KUZALISHA PESA YAKO.

Sehemu sahihi ya kuwekeza pesa yako lazima iwe na sifa kuu zifuatazo

- 1) Usalama wa mtaji wako
- 2) Mrejesho shindani
- 3) Ukwasi (urahisi wa kupata pesa yako)

USALAMA WA MTAJI WAKO

Kitu cha kwanza cha kuhakikisha kabla haujaweka pesa yeko sehemu yoyote ile ni usalama wa hilo eneo, itakuwa kitu ambacho sio cha busara umetafuta hela kwa jasho na unaenda kuipoteza kwa kuwekeza sehemu ambayo haina usalama, ninajua watu wengi ambao wamepoteza pesa zao kwa kuwekeza katika kampuni za wizi (scam).

MREJESHO SHINDANI

Baada ya kuhakikisha kuwa eneo hilo ni salama na unaweza kuwekeza, kitu cha pili ni faida (je faida ni kiasi gani?) sio kitu cha busara kuweka pesa yako sehemu ambayo inatoa riba ya 1% au 2% wakati kuna maeneo unaweza kupata riba mpaka 12% kwa mwaka na kuna usalama.

UKWASI WA UWEKEZAJI

Kitu cha mwisho ni kuangalia urahisi wa namna ambavyo pesa yako (mtaji na faida) inaweza kukufikia, kuna maeneo ambayo ukiwekeza japo faida ipo ila sio rahisi kutoa pesa yako endapo unataka kutoa fedha yako, mfano kuna watu waliwekeza katika baadhi ya hisa na mwisho wa siku walipotaka kuuza hisa zao kukawa hakuna mteja wa kununua na ikawa shida kwao kupata pesa zao kwa wakati.

Uwekezaji ambao tunauzungumzia hapa una sifa zote hizi

SEHEMU YA KWANZA

UWEKEZAJI WA PAMOJA NI NINI?

UTT AMIS ni mfuko wa uwekezaji wa pamoja (mutual fund) ili uweze kuelewa UTT AMIS inavyofanya kazi basi inabidi kuelewa jinsi uwekezaji wa pamoja unavyofanya kazi. Kama unahitaji kuwekeza eneo lolote lile jitahidi kujua wao wanatengeneza faida kwanza, kwani nimekutana na watu wengi ambao wametapeliwa kwa kuwekeza sehemu ambazo hawajui zinafanyaje kazi.

MFANO

Naomba nitoe mfano halisi wa maisha ya kawaida ambao unaeleweka, chukulia kuna kiwanja ambacho kinauzwa kwa bei ya TSH 10 Milioni, na wewe kwa wakati huo unaweza kuwa hauna pesa taslim milioni 10 mfukoni (tuchukulie ya kuwa una milioni 1), sasa unachoweza kufanya ni kutafuta marafiki zako ambao pia wana TSH milioni moja au kiwango chochote cha pesa na kukusanya pesa hiyo na kwenda kununua kiwanja, tuchukulie umepata marafiki zako wengine 9 ambao kila mmoja wao ana TSH 1 milioni, mkijumlisha inapatikana 10 milioni, sasa mpaka hapa mmeshafikisha 10 milioni na mnaweza kwenda kununua kiwanja.

Kumbuka hiki kiwanja ambacho mtanunua kina umiliki wa watu 10 ambao ndio wamechangia pesa yao kununua, sasa tuchukulie baada ya miaka 3 bei ya kiwanja imepanda na kufikia 20 milioni na mkaona ni busara kuuza kwa bei hii, baada ya kuuza, pesa itakayopatikana itagawanywa kwa kila mmoja kulingana na kiasi ambacho amewekeza, na kwa mfano wetu kwa kuwa mmewekeza TSH 1 milioni

kila mmoja na mlikuwa 10, basi ina maana kama mmeuza 20 milioni kila mmoja atapata 2 milioni. Hapa tunasema kiwanja hiki kilikuwa uwekezaji wa pamoja na kama ulivyoona aina hii ya uwekezaji imewawezesha kuwekeza katika kitu ambacho kama ungekuwa peke yako ingekuwa ngumu kuwekeza.

Sasa tunapozungumzia uwekezaji wa pamoja unakuwa hauna tofauti na mfano ambao nimeutoa hapo juu, hapa kunakuwa na meneja wa uwekezaji wenu, baada ya kupokea pesa basi yeye anaenda kuiwekeza kitaalamu kwa niaba yenu na faida ikipatikana inakuja mikononi mwenu.

BAADA YA MENEJA KUKUSANYA PESA ANAWEKEZA WAPI?

Sasa pesa inapopokelewa na meneja wa mfuko ambaye ni UTT AMIS ina kwenda kuwekezwa katika masoko ya mitaji mfano hati fungani na hisa au masoko ya fedha mfano katika akaunti maalumu za benki (fixed account).

Sasa kinachotokea ni kuwa faida ikipatikana katika haya masoko basi inagawanywa kwa kila muwekezaji kulingana na kiasi ambacho amewekeza

Kwa hiyo unaweza kuona ya kuwa hata kama kiasi chako ni kidogo kuwekeza katika hati fungani moja kwa moja kupitia uwekezaji wa pamoja unaweza kuwekeza katika hati fungani au kama uelewa wako wa soko la hisa sio mkubwa unaweza kuwekeza katika soko la hisa kwa njia ya uwekezaji wa pamoja.

UTTT AMIS NI NINI?

UTT AMIS ni kifupi cha Unit Trust of Tanzania Asset Management and Investor Services. Hii taasisi ni meneja wa mifuko sita mpaka sasa, kazi yake ni kupokea pesa kutoka kwa wawekezaji wakubwa na wadogo na kuwekeza katika masoko ya fedha na mitaji, pia kusimamia uwekezaji, taasisi hii iliazishwa mwaka 2003 chini ya jina Unit trust of Tanzania (UTT), na mwaka 2013 ilibadilishwa jina na kuitwa UTT AMIS. Taasisi hii ipo chini ya wizara ya fedha kwa hiyo unaweza kuona kuna usalama wa kuwa taasisi hii haiko chini ya miliki ya watu binafsi bali iko chini ya serikali.

MIFUKO ILIYO CHINI YA UTT AMIS

UTT AMIS ina mifuko sita ambayo ina sifa tofauti tofauti kama tutakavyoona hapo mbele, nayo ni.

- 1) MFUKO WA UMOJA (UMOJA FUND).
- 2) WEKEZA MAISHA (INVEST LIFE)
- 3) MFUKO WA WATOTO (WATOTO FUND)
- 4) MFUKO WA JIKIMU (JIKIMU FUND)
- 5) MFUKO WA UKWASI (LIQUID FUND)
- 6) MFUKO WA HATI FUNGANI (BOND FUND)

Sasa wewe kama muwekezaji unaweza kuwekeza katika mfuko wowote ule kati ya mifuko sita hapo juu ikiwa umekidhi masharti na vigezo vya mfuko husika. Kila mfuko unajitegemea na unaweza kuwekeza katika mfuko mmoja au mifuko yote kama umekidhi vigezo.

NI KIVIPI UTT AMIS NI FURSA YA UWEKEZAJI

UTT AMIS inakupa nafasi ya kuwekeza pesa kwa kima cha chini ch 5000/= kwa baadhi ya mifuko, na hii pesa yako inaenda kuwekezwa katika masoko ya fedha au masoko ya mitaji na unapokea faida pale ambapo mfuko unapokea faida kutoka sehemu ambapo mfuko umewekeza. Na ubora wake ni kuwa faida ya hii mifuko huwa ni ya mara kwa mara na sio lazima usubiri mpaka mwisho wa mwaka kupokea faida, unaweza kuanza kuwekeza hela kesho au baada ya siku kadhaa tayari ukawa umeanza kuona faida.

KIPANDE NI NINI?

Utasikia neno kipande au vipande mara kadhaa, huu ni umiliki ambao muwekezaji anakuwa nao endapo anakuwa amewekeza katika mfuko husika, uwekezaji mzima wa mfuko unagawanywa kwenye sehemu ndogo ndogo, mfano mfuko unaweza kuwa na ukubwa wa BILIONI 200, sasa huu mfuko unagawanywa katika visehemu vidogo vidogo vya thamani ya TSH 100,(hii bei ya vipande inaongezeka kadri mfuko unavyo pata faida) na hivi ndio vinaitwa vipande au kipande. Kwa hiyo ukinunua vipande 10 katika mfuko huu ina maana katika hii bilioni 200 wewe umechangia 1000/= na faida yako itakuwa sawa na idadi ya vipande vyako.

JINSI FAIDA INVYOKUFIKIA KAMA UMEWEKEZA UTT AMIS

Kuna namna mbili za kupata faida kama unakuwa umewekeza UTT AMIS.

1) KUPITIA GAWIO

Kuna mifuko ambayo inawanufaisha wawekezaji wake kwa kupitia njia ya gawio, hapa nina maana kuwa baada ya mfuko kuwa umewekeza pesa na ukapata faida basi unakuwa na utaratibu wa kutoa gawio (sehemu ya faida) kwa wewekezaji wake.

MFANO

Chukulia wewe na rafiki yako mna biashara ambayo mnaifanya kwa pamoja na baada ya kupata faida mkaamua kugawana ile faida kila mmoja wenu kulingana na umiliki wake, sasa hii pesa iliyopatikana kama faida ambayo mmeamua kugawana ndio inaitwa GAWIO.

Kuna mifuko miwili tu mpaka sasa ambayo inatoa gawio nayo ni **MFUKO WA JIKIMU** na **HATI FUNGANI**. Gawio huwa linatolewa kwa vipindi tofauti tofauti, kuna gawio kila mwezi na gawio kila baada ya miezi mitatu, miezi sita au kwa mwaka mara moja.

2) KUPITIA UKUAJI WA MTAJI

Hapa kuna baadhi ya mifuko ambayo haitoi gawio ila faida yake unaipata kwa njia ya ukuaji wa mtaji (capital gain).

MFANO

Bei ya kipande huwa inapanda au kushuka, chukulia mfano umenunua kipande kwa bei ya 200/= na baada ya mwaka mmoja bei ikapanda na ikawa 250/= na ukaamua kuuza hapa unapata faida ya 50/=:, sasa hii faida ndio tunaita ukuaji wa mtaji.

MFANO 2.

Chukulia umenunua kiwanja kwa bei ya 1 milioni na baada ya muda bei ikapanda na kufikia 2 milioni na ukaamua kuuza, hapa tunasema njia ambayo umepata faida ni ukuaji wa mtaji (yaani umewekeza kiasi kidogo na ukapata kiasi kikubwa baada ya muda fulani).

Sasa kwa kuwa bei ya vipande vya UTT AMIS inaongezeka kila siku au baada ya muda fulani basi inakuwezesha wewe kupata faida kupitia **UKUAJI WA MTAJI**

Katika kundi hili kuna mifuko minne **UMOJA, WEKEZA, WATOTO** na **MFUKO WA UKWASI**. Mifuko hii haina sera ya kutoa gawio bali muwekezaji anapata faida kwa njia ya ukuaji wa mtaji. Na hapa ukitaka kupata faida yako mkononi basi itakulazimu kuuza vipande vyako baadhi au vyote kutegemea na uchaguzi wako.

FAIDA ZA KUWEKEZA UTT AMIS

1) KIASI KIDOGO KABISA CHA KUWEKEZA.

Kuna baadhi ya mifuko unaweza kuanza kuwekeza ukiwa na 5000/= tu, kama unafahamu ukitaka kuwekeza katika HATI FUNGANI za serikali za muda mrefu kima cha chini cha kuanza kuwekeza ni TSH 1 milioni, wakati hati fungani za muda mfupi ni 500000/= Ila kama una wekeza kupitia mfuko wa HATI FUNGANI basi itakugharimu 50000/= kama kima cha chini cha kuanzia.

2) HAUHITAJI UJUZI MWINGI KUWEKEZA

Ukitaka kuwekeza katika soko la hisa kwa faida utahitaji kuwa na ujuzi wa kutosha wa kujua kampuni gani uwekeze na pia unatakiwa kuwa na muda wa kusimamia uwekezaji wako ila kupitia UTT AMIS unaweza kuwekeza katika hisa bila kuwa na ujuzi wowote kwani MENEJA wa mfuko ndio anafanya kazi zote hizi kwa niaba yako.

3) UWEKEZAJI MSETO (DIVERSIFICATION).

Chukulia una 5000/= ya kuwekeza na unataka ufanye uwekezaji wa mseto unadhani suala hili linawezekana? au hata kama una 100000/= itakuwa ngumu kufanya uwekezaji mseto. **UWEKEZAJI MSETO** maana yake ni kile kitendo ambacho muwekezaji anakifanya kwa ajili ya kupunguza hasara endapo eneo moja ambalo amewekeza linakuwa halina faida, mfano unaweza kuwekeza katika hisa za CRDB, NMB, DSE ili kwamba ikitokea kampuni moja imefanya vibaya kampuni nyingine zitaendelea kubeba uwekezaji wako.

Ukiwa na kiasi kidogo cha fedha inakuwa ngumu kufanya uwekezaji mseto ambao una tija ila kwa kiasi hiki hiki ukiwekeza katika mfuko wa UTT AMIS ambao ndani yake kuna hisa za makampuni tofauti tofauti na pia umewekeza katika hati fungani unakuwa na uwekezaji mseto wenye maana.

4) UKWASI (LIQUIDITY)

Kama umewekeza katika hisa utafahamu ya kuwa kuna baadhi ya hisa za makampuni hazina wateja wengi kwa baadhi ya vipindi, kwa hiyo unaweza kukaa muda mrefu bila kuuza hisa zako endapo unataka kufanya hivyo, tunapozungumzia UKWASI tuna maanisha ule uwezo wa kubadilisha mali yako au uwekezaji wako kuwa pesa, mfano ukiwa na nyumba unataka kuuza unaweza kukaa siku, miezi au mwaka bila kupata mteja ila ukiwa na dhahabu ni rahisi kupata mteja.

Sasa ukiwa na vipande vya UTT AMIS unakuwa na uhakika wa kuviuza siku yoyote ile unayotaka na pesa yako unaipokea ndani ya siku 3 za kazi kwa baadhi ya mifuko na mifuko mingine utapokea pesa yako baada ya siku 10 za kazi, huu

uhakika hauwezi kuwa nao kama umewekeza katika hisa au hata kama una nyumba yako umepangisha (kwani inaweza kufika muda wa kuchukua kodi na mpangaji wako akawa ana changamoto na usipate pesa yako kwa wakati).

Ukiitaka pesa yako kutoka UTT AMIS, utaipata ndani ya siku 3 na baadhi ya mifuko siku 10 za kazi.

5) MREJESHO SHINDANI (COMPETITIVE RETURN)

Kama unakuwa umeweka pesa yako benki ndani ya mwaka mmoja sio ajabu kupokea riba ambayo ni chini ya 3% ila UTT AMIS ina mrejesho ambao ni mzuri ukilinganisha na maeneo mengi ambayo unaweza kuweka pesa yako.

6) RIBA YA KAMPAUNDI (COMPOUND INTEREST)

Kama kuna kitu kimoja kinachofanya UTT AMIS kuwa sehemu bora ya kuwekeza hasa hasa kama wewe ni muwekezaji wa muda mrefu basi ni hii riba ya kampaundi, riba ya kampaundi iko hivi:

MFANO

Chukulia umefuga mbuzi kwako na huyu mbuzi akazaa mwaka wa kwanza jike, mwaka wa pili unakuwa na mbuzi wawili wanaozaa yule wa kwanza na huyu alizaliwa kwa hiyo mwaka unaofuata mbuzi wa kwanza atazaa na mbuzi wa pili atazaa pia.

Riba ya kampaundi iko hivyo hivyo mwaka wa kwanza unapokea riba katika pesa uliyowekeza baada ya hapo hii riba mwaka unaofuata pia ina pokea riba na miaka inayokuja kila riba ambayo unapokea inapokea riba pia.

MFANO.

Ukiwa umewekeza 1000/= kwa riba ya 10% kwa mwaka ila riba hii ni ya kampaundi inakuwa hivi mwaka wa kwanza utapokea 100/= kama riba sasa kama utakuwa haujatoa hii riba uliyopokea mwaka unaofuata hii riba inakuwa sehemu ya mtaji kwa hiyo mwaka wa pili mtaji unakua 1100/= na riba 110/=
mwaka wa tatu mtaji unakuwa 1210/= na unapokea riba ya 121, hivyo hivyo na kuendelea kwa miaka inayokuja.

Lakini kama unakuwa umewekeza katika ambao unatoa riba rahisi (simple interest) ina maana kwa miaka yote riba ambayo utakuwa unapokea ni 100/= kwa miaka yote.

7) UNaweza KUWEKEZA UKIWA POPOTE PALE TANZANIA.

Unaweza kuanza kuwekeza UTT AMIS popote ulipo Tanzania, kwani unaweza kufungua akaunti kwa njia ya simu na ukaanza kuwekeza kwa njia ya simu pia.

8) UNaweza KUTUMIA VIPANDE VYA UTT AMIS KAMA DHAMANA.

Vipande ya UTT AMIS vinaweza kutumika kama dhamana endapo unataka kuomba mkopo

Pia vipande vinaweza kuhamishika kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine. (kwa hiyo siku ya kuzaliwa ya mtu wako wa karibu badala ya kumnunulia zawadi nyingine unaweza kuhamisha baadhi ya vipande vyako na kumpa huyo mtu)

MREJESHO WA UWEKEZAJI

Sasa unapowekeza ile faida ambayo unaipata kwa mwaka au kwa kipindi fulani ndio tunaitwa mrejesho wa uwekezaji, kwa jina lingine unaitwa **RETURN ON INVESTMENT**.

MFANO

Unapoweka pesa benki na ukaambiwa riba ni 3% kwa mwaka hapa wanachomaanisha ni kuwa kwa pesa yoyote ambayo utaiweka basi wao watakupa 3% ya hiyo pesa kama riba, kwa hiyo kwa mtu aliyewekeza 1 milioni atapewa 30000/= kwa mwaka, sasa huu ndio mrejesho wa uwekezaji.

Hapo mbele utasikia mfuko fulani una mrejesho wa 13% kwa mwaka hapa ina maana kama umewekeza katika mfuko huo kwa mwaka huo basi faida yako ni 13% ya kile kiasi ambacho ulikuwa umewekeza. Mfano kama umewekeza 1 milioni maana yake 130000/= (laki moja na elfu thelathini) ndio faida yako kwa mwaka huo.

SHEHEMU YA PILI

MUONGOZO WA MIFUKO

MGAWANYIKO WA MIFUKO YA UTT AMIS

Mifuko ya UTT AMIS imegawanyika katika makundi mawili kutegemea sera ya maeneo ambayo mifuko hii inatakiwa kuwekeza.

1) MIFUKO YENYE SERA YA KUWEKEZA KATIKA HISA

Hapa kuna mifuko minne ambayo ina sera ya kuwekeza katika hisa kwa kiasi fulani cha uwekezaji wake. Mifuko yenye sera ya kuwekeza katika hisa ni:

- 1) MFUKO WA UMOJA**
- 2) MFUKO WA WEKEZA MAISHA**
- 3) MFUKO WA WATOTO**
- 4) MFUKO WA JIKIMU**

2) MIFUKO AMBAYO HAINA SERA YA KUWEKEZA KATIKA HISA

Hapa tuna mifuko miwili ambayo haina sera ya kuwekeza katika hisa nayo ni:

- 1) MFUKO WA UKWASI**
- 2) MFUKO WA HATI FUNGANI**

Tofauti kubwa ya hii mifuko ni sera (policy) ya maeneo ambayo mifuko hii inatakiwa kuwekeza ila tofauti nyingine ni mapato, mifuko ambayo haina sera ya kuwekeza katika hisa inakuwa na mapato ya kutabirika (predictable income) na pia usalama mkubwa wa mtaji wako. ila mapato yanayotoka katika hisa hayana uwezo wa kutabirika.

Ni kitu cha msingi kujua kabla haujachagua mfuko wa kuwekeza.

MFANO

Chukulia unafanya kazi kwa mabosi wawili, bosi wa kwanza anakulipa mshahara kulingana na hali yake ya ki uchumi siku uchumi ukiwa mzuri anakulipa kiasi kikubwa ila siku uchumi ukiwa vibaya anakulipa kiasi kidogo au hakuna malipo kabisa, bosi wa pili yenye anakulipa mshahara ule ule kwa vipindi vyote na hata kama ukipungua au kuongezeka sio kwa kiasi kikubwa., bosi wa kwanza ni kama mifuko iliyowekeza katika hisa na bosi wa pili ni kama mifuko isiyo na sera ya kuwekeza katika hisa.

MFUKO WA UMOJA



UTANGULIZI

Mfuko huu ndio wa kwanza kabisa kuanzishwa na ulianzishwa mwaka 2005, mfuko huu ni moja kati ya mifuko ambayo ina sera ya kuwekeza katika hisa, sera ya kuwekeza katika hisa ni kuwa uwekezaji hautakiwi kuzidi 50% ya thamani ya mfuko.

NAMNA YA KUPATA FAIDA

Mfuko huu hauna sera ya kutoa gawio kwa hiyo muwekezaji anapata faida kupitia ukuaji wa mtaji, mfano umenunua kipande 100 na baada ya muda kipande kikaongezeka bei na kuwa 140/= basi faida yako hapa ni 40/=, katika mfumo huu ili muwekezaji aweze kupata faida mkononi basi itambidi auze vipande baadhi au vyote kulingana na uchaguzi wake.

ANAYESTAHILI KUWEKEZA

Mfuko huu unampa nafasi mtanzania yoyote kuwekeza, pia taasisi yoyote ile inaruhusiwa kuwekeza huku.

KIASI CHA CHINI CHA KUWEKEZA

Hapa kiasi cha chini cha kuanza kuwekeza ni vipande 10 bila kujali bei ya kipande, mfano kama bei ya kipande kwa siku hiyo ni 800/= na wewe unataka kuanza kuwekeza katika mfuko huu basi unatakiwa kuwa na 8000/= na pia uwekezaji wa nyongeza (kama unataka kuongeza kununua vipande) ni vipande kumi na hakuna ukomo wa idadi ya vipande ambavyo unaweza kununua. Unaweza kununua mara nyingi uwezavyo.

GHARAMA ZA KUNUNUA NA KUUZA KIPANDE.

Hapa kama unataka kununua kipande hakuna gharama yoyote ambayo unakatwa, kama kipande kinauzwa 800/= basi utanunua kwa bei hii hii. Ila kama unataka kuuza vipande vyako basi utakatwa 1% ya vipande ambavyo unauza, mfano kama unauza vipande vyenye thamani ya 100000/= basi utakatwa 1000/= (hii ndio 1% ya thamani ya vipande vyako unavyouza).

MUDA WA ZUIO

Huu ni muda ambao unazuiliwa kutoa pesa zako, kuna baadhi ya mifuko ina zuio la muda, kwamba ukiwekeza huko hautaruhusiwa kuchukua pesa zako mpaka muda wa zuio uishe. Mfuko wa UMOJA hauna muda wa zuio. Unaweza kununua na kuuza vipande muda wowote.

KUUZA VIPANDE

Unaruhusiwa kuuza vipande siku yoyote ile ambayo UTT AMIS imefungua ofisi zao, na pia unaruhusiwa kuuza vipande vyako kwa idadi yoyote ile unayoitaka mfano kama una vipande 1000 unaweza kuamua kuuza vipande vyote au ukaamua kuuza kiasi tu cha vipande vyako. Baada ya kuuza vipande pesa itakufikia ndani ya siku 10 za kazi.

MREJESHO WA MFUKO HUU

Mfuko huu una sera ya kuwekeza katika hisa, kwa hiyo mapato yake huwa yanabadilika kutokana na utendaji kazi wa soko la hisa, ila kihistoria toka mfuko huu unaanzishwa mpaka mwaka 2021 mrejesho wake ulikuwa wa wastani wa 13.2%

Umoja Fund Performances for the Financial Year Ending June															
FY/Return	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020
Return [%]	9.9	8.8	21.2	7.3	7.4	8.2	14.5	15.9	51.6	18.2	7.2	6.6	14.4	-1.2	10.3
3 Month Period, ending December 2020 [%]															14.4
1 Year Period, ending December 2020 [%]															12.4
5 Years Period, ending December 2020 [%]															7.4
Since Inception [%]															13.2

Hapo juu ambapo imeandikwa return % ndio mrejesho wa kila mwaka kwa miaka iliyopita.

KUHAMISHA VIPANDE AU KUVITUMIA KAMA DHAMANA

Vipande ya mfuko wa umoja vinaweza kuhamishwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine na pia vipande vinaweza kutumika kama dhamana pindi unapotaka kuomba mkopo katika taasisi ya fedha.

MFUKO WA WEKEZA MAISHA



UTANGULIZI

Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2007 na ni moja kati ya mifuko minne ambayo ina sera ya kuwekeza katika soko la hisa. Huu mfuko una faida za aina mbili, faida ya kwanza ni faida ya uwekezaji na faida ya pili ni faida ya bima. Mfuko huu una lengo la kumsaidia muwekezaji kuwekeza kitaalamu na kwa utaratibu maalumu, hii ni moja kati ya tofauti kati ya mfuko huu na mifuko mingine. Uwekezaji katika mfuko huu pia una kikomo cha muda, ambapo uwekezaji unadumu kwa miaka 10 tu.

Unapowekeza katika mfuko huu unakuwa na faida za namna mbili

- 1) uwekezaji
- 2) bima

JINSI YA KUPATA FAIDA

Mfuko huu haulipi gawio, kwa hiyo muwekezaji anapata faida kwa ukuaji wa mtaji (capital gain), na faida ya pili ni bima na hapa katika bima kuna bima za aina mbili, bima ya maisha na bima ya ulemavu wa kudumu pia kuna bima ya ajali binafsi (tutaona hapo chini inakuwaje)

KIASI CHA CHINI CHA KUWEKEZA

Katika mfuko huu kiasi cha chini kabisa cha kuwekeza kwa muda wote wa miaka 10 ni milioni moja, ila kwa kuwa unaweza kuchangia kila mwezi basi kiasi cha chini cha kuwekeza ni 8340/=

NAMNA YA KUWEKEZA

Mfuko huu una ukomo wa muda wa kuwekeza (miaka 10) baada ya muda huu uwekezaji wako unakuwa umefikia mwisho na unaruhusiwa kuchukua pesa yako yote, au unaweza kuamua kufungua mpango mpya baada ya kuwa hiyo miaka 10 imeisha.

Kabla haujaanza kuwekeza katika mfuko huu utatakiwa kuchagua kiasi ambacho utachangia kwa miaka yote kumi (kiasi ambacho utawekeza kwa muda wote) na baada ya hapo utachagua namna ambavyo utakuwa unachangia hii pesa.

MFANO

Kama umekusudia kuwa ndani ya miaka 10 unataka uwe umewekeza milioni 1 au milioni 100 basi utatakiwa uainishe hiki kiasi kabla haujaanza kuwekeza, na katika kuchagua kiasi ambacho utawekeza kwa miaka yote 10 hakuna kikomo cha pesa ambacho unaweza kuchagua ila baada ya kuchagua ni kiasi gani utawekeza hautaruhusiwa kubadilisha tena mpaka mpango wako huu uishe. Huu ndio utofauti uliopo kati ya mfuko huu na mifuko mingine, mifuko mingine hauchagui kiasi ambacho utawekeza kwa muda wote unaweza kuanza na 5000/= na ukawekeza utakavyo ila mfuko wa WEKEZA haukuruhusu kuwekeza bila kuchagua kiasi ambacho utawekeza kwa muda wote.

NAMNA YA KUCHANGIA

Baada ya kuanisha kiasi ambacho utawekeza kwa miaka yote 10 hatua ya pili ni kuchagua namna ambavyo utachangia hii pesa. Kuna namna mbili za uchangiaji katika mfuko huu.

1) Uchangiaji wa mara moja

Hapa kama umeainisha ya kuwa unataka kuwekeza milioni moja au kiasi chochote kile na ikatokea ya kuwa unacho kile kiasi unaweza kuwekeza kiasi chote kwa mara moja na ukatulia, kumbuka kama umeainisha kuwa utachangia milioni moja au kiasi chochote na ukakitoa kwa mara moja basi hautaruhusiwa kuongeza kiasi chochote tena mpaka mpango wako uishe.

2) Uchangiaji wa mara kwa mara

Hapa baada ya kuanisha kiasi ambacho utakuwa unachangia kwa muda wote wa uwekezaji wako ila ikatokea ya kuwa unataka kuwa unachangia kiasi kidogo kidogo basi unaweza kuchagua uchangiaji wa mara kwa mara. Hapa katika uchangiaji wa mara kwa mara unaweza kuchagua kuchangia kila mwezi, kila miezi sita au kila mwaka.

MFANO

Chukulia umeainisha ya kuwa kwa miaka yote 10 utachangia milioni moja ila hiyo pesa ukaainisha kuwa utakuwa unachangia kila mwezi basi itakubidi kuwa unachangia 8340/= (kama unachangia kiasi hiki kwa mwezi basi baada ya miaka 10 utakuwa umetimiza milioni 1).

MFANO 2

Chukulia umeainisha kuwa kwa miaka yote 10 utawekeza milioni 1 ila hiyo pesa ukaamua ya kuwa utakuwa unachangia kila miezi sita basi itakubidi kuwa unachangia 50000/= kila baada ya miezi sita.

MFANO 3

Chukulia umeainisha kuwa kwa miaka yote 10 utawekeza milioni 1 ila hiyo pesa ukaamua ya kuwa utakuwa unachangia kwa mwaka mara moja basi itakubidi kuwa unachangia 100000/= kila mwaka.

Unachotakiwa kukifanya ni kuchukua pesa ambayo umeanisha ya kuwa utakuwa unachangia na kugawanya kwa 120 kama utakuwa unachangia kila mwezi (kwani ndani ya miaka 10 kuna miezi 120) ili kujua kiasi ambacho unatakiwa kuchangia, na kama unataka kuchangia kila baada ya miezi sita basi gawanya kwa 20 (utapata pesa ambayo unatakiwa kuchangia kila baada ya miezi sita), na kama unataka kuchangia kila mwaka basi gawanya pesa yako kwa 10 na utapata jibu.

ANAYESTAHILI KUWEKEZA

Hapa mtu ambaye anastahili kuwekeza ni mtanzania mwenye umri wa miaka 18 mpaka 55.

MUDA WA ZUIO

Hapa kuna zuiro la miaka mitano (5) hapa ina maana kama umewekeza katika mfuko huu basi hautaruhusiwa kutoa pesa yako mpaka baada ya miaka 5, ila baada ya miaka 5 unaruhusiwa kutoa pesa yako mpaka 75% na iliyobakia utaweza kutoa baada ya mpango wa miaka 10 kuwa umeisha.

MAKATO WAKATI WA KUNUNUA NA KUUZA

Hakuna makato wakati wa kununua vipande ila kama utatoa pesa yako baada ya zuiro la miaka 5 basi utakatwa 2% ya vipande ambavyo unauza ila kama ukisubiri mpaka baada ya miaka 10 hakuna makato yoyote.

MREJESHO WA MFUKO

Mfuko huu una sera ya kuwekeza katika hisa ila kihistoria mfuko huu toka uanzishwe 2007 una wastani wa mrejesho wa 13.2%.

Wekeza Maisha Fund Performances for the Financial Year Ending June													
FY/Return	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020
Return [%]	11.0	13.0	9.1	11.0	12.0	12.0	25.0	11.3	3.0	6.4	8.4	11.1	24.0
3 Month Period, ending December 2020 [%]													16.6
1 Year Period, ending December 2020 [%]													24.6
5 Years Period, ending December 2020 [%]													12.3
Since Inception [%]													13.2

Huo ni mrejesho wa mfuko wa WEKEZA kwa miaka iliyopita, sehemu iliyoandikwa FY ni mwaka husika, na sehemu iliyoandikwa return ndio mrejesho wake, mfano mwaka 2008 mfuko ulikuwa na mrejesho wa 11% kama ulikuwa umewekeza huku maana faida yako ingekuwa 11% ya kiasi ulichowekeza.

FAIDA YA BIMA

Katika faida ya bima kuna bima za aina mbili

Bima ya maisha na ulemavu wa kudumu pamoja na bima ya ajali binafsi pamoja.

1) Bima ya maisha na ulemavu wa kudumu

Hapa malipo ya bima yanategemea mpango ambao umechagua wa jinsi ya kuchangia

a) Mpango wa kuwekeza mara moja

Kama umechagua mpango wa kuwekeza mara moja, na ikatokea kifo au ulemavu wa kudumu basi fidia ya bima itakuwa sawa sawa na kiasi ambacho umechangia, mfano kama umechangia milioni 10 na ikatokea umepata matatizo basi fidia ya bima itakuwa 10 milioni, kama katika mpango wako uliwekeza 20 milioni basi faida hii itakuwa 20 milioni pia ila kama kiasi ambacho umewekeza kinazidi 25 milioni basi fidia itakuwa 25 milioni tu (kwani 25 milioni ndio kikomo cha fidia ya bima). Katika mpango huu hakuna fidia ya bima mwaka wa kwanza isipokuwa kifo cha muwekezaji kiwe ni kwa ajali.

b) Mpango wa kuwekeza mara kwa mara

Katika mpango huu fidia inakuwa sawa sawa na kiasi ambacho bado haujachangia kwenye mpango wako.

MFANO

Kama mpango wako umeanisha kuwa utachangia milioni 10 na ukapata changamoto wakati ambao umeshachangia 3 milioni basi fidia yako itakuwa sawa na kile kiasi ambacho haujachangia kwenye mpango wako na kwa mfano wetu itakuwa 7 milioni. Ila ukomo wa fidia hapa pia ni milioni 25, mfano kama mpango wako umeanisha utachangia 100 milioni ila ukapata changamoto umechangia milioni 30 tu basi fidia yako itakuwa 25 milioni. Katika mwaka wa kwanza hapa hakuna fidia na katika mwaka wa 10 hakuna fidia kama muwekezaji

amechagua mpango wa kuwekeza mara moja kwa mwaka. Pia fidia itatoka mwaka wa kwanza kama chanzo cha matatizo ni ajali.

2) Bima ya ajali binafsi (personal accident)

Kikomo cha pesa ambayo inalipwa hapa ni 5 milioni.

Kumbuka kutokana na kuwa vipande vimeunganishwa na bima vipande vya mfuko huu haviwezi kuhamishwa au kutumiwa kama dhamana.

MFUKO WA WATOTO.



UTANGULIZI

Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2008 ukiwa na lengo la kumsaidia mtoto wa kitanzania katika masomo.

MPANGO WA KUPATA FAIDA

Mfuko huu haulipi gawio kwa hiyo muwekezaji anapata faida kupitia ongezeko la mtaji (capital gain).

ANAYESTAHILI KUWEKEZA

Mtu yoyote au taasisi yoyote inaruhusiwa kuwekeza kwa niaba ya mtoto wa kitanzania ambaye hajafikisha umri wa miaka 18.

KIASI CHA CHINI CHA KUANZA KUWEKEZA

Kiasi cha chini cha kuanza kuwekeza katika mfuko huu ni 10000/= na kama utataka kuongeza tena uwekezaji wako kiasi cha chini ni 5000/= hapa maana yake ni kuwa kama ndio unataka kuwekeza kwa mara ya kwanza basi utatakiwa kuwa na kima cha chini cha 10000/= na baada ya hapo kama ukitaka kuongeza

uwekezaji wako basi kima cha chini ni 5000/= ila unaweza kuwekeza kiasi chochote kile utakacho bila kikomo na mara nyingi unavyoweza.

GHARAMA YA KUNUNUA NA KUUZA VIPANDE

Ukitaka kununua vipande katika mfuko huu hakuna gharama yoyote ile ila kama ukitaka kuuza vipande basi kama ni ndani ya miaka 3 toka ulipoanza kuwekeza basi utakatwa 1% ila baada ya miaka 3 hakuna makato ya aina yoyote. Pia kuna unafuu wa watoto wenye ulemavu au watoto yatima wao hakuna makato yoyote.

MUDA WA ZUIO

Hapa hautaruhusiwa kuuza vipande au kutoa pesa mpaka pale ambapo mtoto anakuwa amefikisha umri wa miaka 12 na hapo unaweza kuuza vipande baadhi au vipande vyote ila unaweza kutoa pesa hata kama mtoto hajafikisha umri wa miaka 12 kama kuna sababu za msingi kama pesa ya matibabu ya mtoto.

Pia kuna ukomo wa uwekezaji pindi mtoto anapofikisha miaka 24 basi uwekezaji wake unakuwa umefikia mwisho na anaweza kutoa pesa yake yote au kuhamia mfuko mwingine au akafungua mpango mwingine kwa mtoto mwingine na yeye akawa kama mzazi au mlezi wa huyu mtoto.

JINSI FAIDA INAVYOWEZA KUMFIKIA MTOTO

Mtoto anaweza kufaidika kwa namna mbili

1) Kupitia ufadhili wa masomo (scholarship)

Hapa mtoto anakuwa analipiwa pesa na UTT AMIS moja kwa moja katika eneo ambalo mzazi amesainisha, na hii inaweza kulipwa mara moja kwa mwaka au mara mbili kwa mwaka kutokana na uchaguzi wa mzazi au mlezi.

2) Kupitia ongezeko la mtaji

Hapa UTT AMIS hawatalipa kitu chochote kile ila muwekezaji atapata faida kupitia ukuaji wa mtaji.

MREJESHO WA MFUKO

Mfuko huu una sera ya kuwekeza katika hisa, kwa hiyo mapato yake yanategemea utendaji kazi wa soko la hisa ila kwa wastani toka mfuko unaanzishwa mrejesho wa mfuko huu ni 12.3%.

Watoto Fund Performances for the Financial Year Ending June												
FY/Return	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020
Return [%]	6.0	10.0	13.0	13.0	12.0	31.0	11.3	3.0	6.4	8.4	11.1	24.0
3 Month Period, ending December 2020 [%]												13.1
1 Year Period, ending December 2020 [%]												14.4
5 Years Period, ending December 2020 [%]												7.7
Since Inception [%]												12.3

Huo ni mrejesho wa mfuko wa WATOTO kwa miaka iliyopita, sehemu iliyoandikwa FY ni mwaka husika, na sehemu iliyoandikwa return ndio mrejesho wake, mfano mwaka 2009 mfuko ulikuwa na mrejesho wa 6% kama ulikuwa umewekeza huku maana yake ni kuwa faida yako ingekuwa 6% ya kiasi ulichowekeza.

MENGINEYO.

Vipande vinaruhusiwa kutumika kama dhamana kama unataka kuchukua mkopo kama mnufaika wa mkopo ni mtoto, pia unaruhusiwa kuhama mfuko huu kwenda mwingine.

MFUKO WA JIKIMU



UTANGULIZI

Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2008, ukiwa na lengo la kumsaidia muwekezaji wa kitanzania kupata mapato ya mara kwa mara kupitia GAWIO, huu mfuko una sera ya kuwekeza katika hisa, pia ni mfuko ambao muwekezaji anapata faida kwa njia ya gawio na ukuaji wa mtaji.

Jinsi ya kuwekeza katika mfuko huu

Mfuko huu una mipango mitatu ambayo muwekezaji anaweza kuchagua

- 1) Mpango wa gawio kila baada ya miezi 3**
- 2) Mpango wa gawio kila mwaka**
- 3) Mpango wa kukuza mtaji (reinvestment option)**

Ukichagua mpango wa gawio kila baada ya miezi 3 na kama umetimiza vigezo basi utakuwa unapokea gawio kila baada ya miezi 3, na kama ni gawio kila mwaka basi utakuwa unapokea gawio kila mwaka. Na kama umechagua mpango wa kukuza mtaji basi utakuwa haupokei gawio lako mkononi ila pesa yako inatumika kukununulia vipande.

ANAYESTAHILI KUWEKEZA.

Mfuko huu uko wazi kwa mtanzania yoyote yule kuwekeza.

KIASI CHA CHINI CHA KUANZA KUWEKEZA

Kiasi cha chini cha kuanza kuwekeza kinategemea mpango ambao umeuchagua, kwa mpango wa kupata gawio kila baada ya miezi 3 basi kima cha chini cha kuanza kuwekeza ni 2 milioni, kwa mpango wa gawio kila mwaka kima cha chini cha kuanza kuwekeza ni 1 milioni, katika mipango hii miwili kama unataka kufanya uwekezaji wa nyongeza basi kima cha chini 15000/= (hapa maana yake ni kuwa baada ya kuwa umetoa hiyo 2 milioni ila ukataka kuongeza kiasi kingine basi kiasi cha chini ndiyo 15000/= na mpango wa kukuza mtaji kima cha chini cha kuanza kuwekeza ni 5000/= na pia kama unataka kufanya uwekezaji wa nyongeza ni 5000/= katika mpango huu. Katika mipango yote hakuna ukomo wa kiasi ambacho muwekezaji anaweza kuwekeza.

GHARAMA ZA KUNUNUA NA KUUZA.

Ukitaka kununua kipande hakuna makato ya aina yoyote, ila kama ukitaka kuuza kipande ndani ya mwaka mmoja wa uwekezaji wako basi utakatwa 2% ya pesa unayouzia, ukitaka kuuza vipande vyako ndani ya mwaka wa pili basi utakatwa 1.5% ya pesa unayouzia na kama ukitaka kuuza ndani ya mwaka wa tatu basi makato ni 1% ila baada ya hiyo miaka hakuna makato endapo unataka kuuza vipande.

MUDA WA ZUIO

Mfuko huu hauna zuio, muwekezaji anaweza kuuza baadhi au vipande vyote muda wowote.

MREJESHO WA MFUKO

Mfuko huu umewekeza katika hisa kwa hiyo mapato yake huwa yana badilika kulingana na utendaji kazi wa soko la hisa.

KUMBUKUMBU

Ukiwekeza katika mfuko wa Jikimu sio kwamba ukiwa na milioni 2 basi utawekwa katika mpango wa gawio kila baada ya miezi mitatu moja kwa moja hapana, unaweza kuwekeza kiwango chochote kile na ukachagua mpango wa kukuza mtaji.

GAWIO

Gawio huwa linatolewa kulingana na utendaji wa kazi wa mfuko, kuna mwaka gawio linaweza kuwa kubwa na kuna mwaka gawio linaweza kupungua au hakuna gawio, ila ni matarajio ya meneja wa mfuko kutoa gawio kila mwaka ila kutokana na hali ya uchumi kuwa tofauti hata hali ya gawio inaweza kubadilika pia ila kihistoria mfuko umekuwa ukilipa gawio kwa miaka yote.

Jikimu Fund Performances for the Financial Year Ending June												
FY/Return	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020
Return [%]	22.0	18.0	17.0	21.0	17.0	41.0	16.2	4.0	9.6	10.0	10.6	15.6
ID Per Unit	12.0	12.0	12.0	12.0	12.0	16.0	9.0	12.0	12.0	12.0	12.0	12.0
3 Month Period, ending December 2020 [%]												15.0
1 Year Period, ending December 2020 [%]												17.4
5 Years Period, ending December 2020 [%]												9.5
ID Paid Per Unit												12.0
Since Inception [%]												8.4

Huo ni mrejesho wa mfuko wa JIKIMU kwa miaka iliyopita, sehemu iliyoandikwa FY ni mwaka husika, na sehemu iliyoandikwa return ndio mrejesho wake, na sehemu iliyoandikwa ID (income distribution) ndio gawio kwa mwaka husika. mfano mwaka 2009 mfuko ulikuwa na mrejesho wa 22% kama ulikuwa umewekeza huku maana faida yako ingekuwa 22% ya kiasi ulichowekeza, lakini pia Gawio kwa kila kipande lilikuwa 12 kwa mwaka huo.

Kama unavyoona kwa miaka yote Gawio limekuwa likitoka na mwaka 2015 gawio lilipungua na kuwa TSH 9, huku mwaka 2014 gawio liliongezeka na kuwa TSH 16/= kwa kipande.

MFUKO WA UKWASI



UTANGULIZI

Mfuko wa ukwasi ni moja kati ya mifuko ambayo haina sera ya kuwekeza katika hisa. mfuko huu unampa nafasi muwekezaji kuwekeza pesa kwa muda mrefu au mfupi huku akipata usalama wa mtaji wake na pia urahisi wa kuchukua pesa yake endapo **atahitaji kufanya hivyo**

ENEO AMBALO MFUKO HUU UMEWEKEZA.

Mfuko huu una sera ya kuwekeza katika mapato ya kuaminika katika hati fungani na amana za kibenki, kwa hiyo unaweza kuona kuwa hapa hakuna kupanda na kushuka kwa mtaji wako endapo unakuwa umewekeza huku kama ilivyo katika mifuko iliyowekeza katika hisa.

MPANGO WA KUPATA FAIDA

Mfuko huu haulipi gawio kwa hiyo muwekezaji anapata faida kwa ukuaji wa kipande mfano kama umenunua kipande kwa bei ya 200/= na bei ya kipande ikakua mpaka kufikia 230/= basi hii 30/= ndio faida yako.

ANAYESTAHILI KUWEKEZA HAPA

Mtu yoyote au taasisi inaruhusiwa kuwekeza katika mfuko huu.

KIASI CHA CHINI CHA KUANZA KUWEKEZA

Kiasi cha chini cha kuanza kuwekeza katika mfuko huu ni 100000/= na uwekezaji wa nyongeza kima cha chini ni 10000/=.

GHARAMA YA KUNUNUA AU KUUZA

Hakuna gharama yoyote wakati wa kununua au kuuza.

MUDA WA ZUIO

Hakuna muda wa zuiro unaweza kuuza na kununua vipande siku yoyote ile pia pesa yako unaipokea ndani ya siku tatu tu za kazi.

UKOMO WA UWEKEZAJI

Mfuko huu hauna ukomo wa uwekezaji na pia hakuna kikomo cha pesa ambayo unaweza kuwekeza.

MREJESHO WA MFUKO HUU

Mfuko huu hauna sera ya kuwekeza katika hisa na hivyo mapato yake ni ya kuaminika na hayana mabadiliko kama ilivyo katika hisa. Kihistoria mfuko huu una mrejesho wa kati ya 12- 15% kwa mwaka.

Liquid Fund Performances for the Financial Year Ending June							
FY/Return	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020
Return [%]	11.3	12.8	13.4	15.3	13.7	11.4	15.1
3 Month Period, ending December 2020 [%]							14.4
1 Year Period, ending December 2020 [%]							15.7
5 Years Period, ending December 2020 [%]							15.5
Since Inception [%]							13.3

Huo ni mrejesho wa mfuko wa UKWASI kwa miaka iliyopita, sehemu iliyoandikwa FY ni mwaka husika, na sehemu iliyoandikwa return ndio mrejesho wake, mfano mwaka 2014 mfuko ulikuwa na mrejesho wa 11.3% kama ulikuwa umewekeza huku maana faida yako ingekuwa 11.3% ya kiasi ulichowekeza.

Unaweza kuhama mfuko wa ukwasi kuelekea mfuko wa hati fungani bila gharama za ziada, ila hauwezi kuhama kutoka mfuko huu kwenda mfuko ambao una sera ya kuwekeza katika hisa.

MFUKO WA HATI FUNGANI



UTANGULIZI

Mfuko huu pia hauna sera ya kuwekeza katika hisa. Na lengo la mfuko huu ni kutoa mapato ya mara kwa mara kupitia gawio, mfuko huu ulianzishwa 2019

MPANGO WA KUWEKEZA

Mfuko huu una sera ya kuwekeza katika mapato ya kuaminika, hapa nazungumzia hati fungani au amana za kibenki, hivyo mapato yake ni ya kuaminika.

NAMNA YA KUPATA FAIDA

Katika mfuko huu unaweza kupata faida kwa namna mbili

- 1) Kupitia ukuaji wa mtaji
- 2) Kupitia gawio

MIPANGO YA UWEKEZAJI

Katika mfuko huu kuna mipango mitatu ya uwekezaji, kuna mpango wa gawio kila mwezi, mpango wa gawio kila miezi sita na mpango wa kukuza mtaji (reinvestment).

Katika mipango yote hapo juu unapokea gawio ila utofauti wa mpango wa ukuaji wa mtaji ni kuwa gawio lako haupokea mkononi bali linaenda kukununulia vipande tena.

ANAYESTAHILI KUWEKEZA

Mfuko huu uko wazi kwa muwekezaji yoyote yule kuwekeza binafsi au taasisi.

KIASI CHA CHINI CHA KUWEKEZA

Kiasi cha chini kinategemea mpango ambao umechagua, kama unataka kupokea gawio kila mwezi basi kima cha chini ni 10 milioni, kama unataka gawio kila baada ya miezi sita basi kima cha chini cha kuanza kuwekeza ni 5 milioni, na kama unataka mpango wa kukuza mtaji kima cha chini ni 50000/= na uwekezaji wa nyongeza kwa mipango yote 3 ni 5000/= kumbuka hiki ni kiwango cha chini tu cha kuanzia ila hakuna kikomo cha pesa unachoweza kuwekeza, pia unaweza kuchagua mpango wa kukuza mtaji hata kama pesa yako inatosha kuwa unapokea gawio kila mwezi (maana yangu ni kuwa sio kwamba ukiwa na milioni 10 au zaidi basi utakuwa unalipwa gawio moja kwa moja hapana unaweza kuchagua ukuaji wa mtaji)

GHARAMA YA KUUZA NA KUNUNUA

Hakuna gharama ya kuuza wala kununua ila endapo unauza vipande vyako pesa utaipokea ndani ya siku kumi za kazi.

ZUIO

Mfuko huu una zuiio la miezi mitatu.

Katika mfuko huu hakuna ukomo wa kiasi ambacho unaweza kuwekeza na pia kuna unafuu wa kodi kwa gawio ambalo unapokea, kwani gawio halina makato.

MREJESHO WA MFUKO

Mfuko huu pia umewekeza katika mapato ya kutabirika na kihistoria mfuko huu umekuwa na mrejesho wa kati ya 12% to 15% kwa mwaka, pia kihistoria gawio limekuwa tsh 12 kwa kipande kwa mwaka, ila hii inaweza kubadilika kulingana na utendaji wa mfuko

Annualized Returns [%] as on 30 th September, 2021	
Since Launch [Sept, 2019]	1 Year
15.2%	16.3%

SEHEMU YA TATU

JINSI YA KUSIMAMIA UWEKEZAJI WAKO

JINSI YA KUANZA KUWEKEZA KWA MARA YA KWANZA

Jinsi ya kuanza kuwekeza kwa mara ya kwanza UTT AMIS ni rahisi mno, unachotakiwa ni kufungua akaunti, na kuna njia tatu ambazo unaweza kuzitumia ili kufungua akaunti ya mfuko wowote ule ambao umeuchagua

1) KWA KUTUMIA SIMU YA MKONONI

Hapa utabonyeza *150*82* kisha utafuata maelekezo ya jinsi ya kufungua akaunti katika mfuko wowote ule, na baada ya kufungua akaunti utapewa namba ya kumbukumbu au namba ya akaunti ya uwekezaji ambayo utakuwa unaitumia, na baada ya hapo unaweza kuanza kuwekeza mara moja kama utahitaji kuwekeza kwa njia ya simu, kama utakwama eneo lolote unaweza kuwapigia UTT AMIS simu bure kabisa kwa mawasiliano yaliyo mwisho wa kitabu hiki. Kama ukitumia njia hii kufungua akaunti utaruhusiwa kuwekeza kwa kununua vipande tu ila kama ukitaka kuuza vipande vyako itakubidi kukamilisha usajili na nitakuelekeza hapo chini inakuwaje.

2) KWA KUTEMBELEA TAWI LOLOTE LA CRDB

CRDB ni mwangalizi wa mifuko ya UTT AMIS lakini pia ni wakala wa UTT AMIS, kwa hiyo ukitembelea tawi lolote la CRDB utapata huduma ya kufungua akaunti na kuwekeza pia.

3) KWA KUTEMBELEA OFISI ZA UTT AMIS

Kwa sasa UTT AMIS haina ofisi kila mkoa ila kama uko mkoa wa Dar es salaam, Mwanza, Mbeya au Arusha unaweza kutembelea ofisi za UTT AMIS na unaweza kufungua akaunti hapo na ukaanza kuwekeza.

4) KUPITIA MADALALI WA SOKO LA HISA (STOCKBROKERS)

Madalali wa soko la hisa pia ni mawakala wa UTT AMIS, ukitembelea dalali yoyote yule anaweza kukusaidia kufungua akaunti na pia unaweza kuwekeza kupitia hawa madalali.

5) KUPITIA APLIKESHENI YA UTT AMIS (UTT AMIS APP)

Pia unaweza kufungua akaunti na hata kuanza kuwekeza katika mfuko wa UTT AMIS kupitia aplikesheni hii ya UTT AMIS.

JINSI YA KUKAMILISHA USAJILI

Baada ya kuwa umefungua akaunti kwa njia ya simu hautaruhusiwa kuuza vipande vyako bila kukamilisha usajili, utakacho ruhusiwa ni kuwekeza tu, sasa ili upate nafasi ya kuuza vipande vyako unatakiwa kukamilisha usajili, sasa unaweza kwenda benki ya CRDB, ofisi za UTT AMIS, Madalali wa soko kwa ajili ya kukamilisha usajiri lakini pia unaweza kupakua fomu za kukamilisha usajiri ambazo utazipata katika tovuti ya UTT AMIS ambayo iko mwisho wa kitabu hiki na ukajaza fomu na kuzituma kwa njia ya barua pepe (email). uwekezaji@uttamis.co.tz.

JINSI YA KUUZA VIPANDE VYAKO

Baada ya kuwa umekamilisha usajili wako basi unaruhusiwa kuuza vipande katika mfuko uliowekeza kama umekidhi vigezo vya kuuza, na jinsi ya kuuza ni rahisi mno, unachotakiwa kufanya ni kutembelea tawi lolote la benki ya CRDB ukiwa na kitambulisho chako na pale utapewa fomu ya kujaza na baada ya kujaza fomu basi zoezi la kuuza vipande litafanyika, pia unaweza kuuza vipande kwa kutembelea ofisi za UTT AMIS au Madalali wa soko kwa ajili ya kuuza vipande. Pesa yako utaipata ndani ya muda ambao umeanishwa na UTT AMIS katika mfuko husika mfano kwa mfuko wa UKWASI pesa yako utaipata ndani ya siku 3 kazi.

JUA GHARAMA AMBAZO UNAINGIA WAKATI WA KUWEKEZA

Kuna gharama za aina mbili ambazo unaweza kuingia endapo unakuwa unafanya uwekezaji wa aina yoyote ile.

- 1) Gharama ambazo ziko ndani ya uwekezaji
- 2) Gharama ambazo ziko nje ya uwekezaji

Japokuwa tumeona ya kuwa katika kila mfuko hakuna gharama yoyote ile endapo unakuwa unanunua vipande ila ili kufanikisha zoezi la ununaji vipande kuna gharama ambazo unaweza kuwa unaingia ili kufanikisha zoezi mfano hapo chini wa mtu ambaye anawekeza kwa njia ya simu

Maelezo ya Ankara:

Namba ya kampuni: 167788

Jina la kampuni: UTT AMIS

Kumbukumbu ya malipo: 5000

Kiasi 10,000 Ada: TSh 600

Ingiza namba ya siri kuhakiki:

CANCEL

SEND

Kama unavyoona huyu muwekezaji anataka kuwekeza 10000/= kwa njia ya simu ila gharama ambayo mtandao wanakata ni 600/= ambayo ni sawa na asilimia 6% ya kiasi ambacho anawekeza, sasa kama ulivyoona mrejesho wa mifuko mingi ni kati ya asilimia 12% mpaka 15%, sasa kama unapoteza 6% kama makato wakati wa kuwekeza basi unakua umepoteza faida ya karibuni miezi 6 na hii sio hekima.

Kama unawekeza pesa nyingi makato yanakuwa kidogo na pia kama unawekeza kwa muda mrefu basi hii 6% inaweza isiwe kitu ila kama unaweza kuepuka makato yasiyo ya lazima basi unajiweka katika nafasi ya kuwa na faida nzuri.

Kuna njia ambazo unaweza kuzitumia ambazo hazina gharama kabisa kama kulipia kupitia benki ya CRDB au Madalali wa soko au kuwaona UTT AMIS moja kwa moja ili kuwekeza, sisemi kwamba usiwekeze kwa njia ya simu ila ninachosema ni kuwa kama kuna nafasi ya kuepuka makato yasiyo na lazima basi itumie hiyo vizuri.

JINSI YA KUTOA FAIDA NA KUBAKIZA MTAJI

Ukiwekeza UTT AMIS unapata nafasi ya kujua idadi ya vipande unavyomiliki na thamani yake, sasa wewe kama muwekezaji jukumu lako ni kutunza kumbukumbu ya pesa kiasi gani umewekeza ili kujua ni faida kiasi gani umepokea, mfano kama umewekeza 100000/= na baada ya miezi miwili mfuko wako ukawa umekua na kufikia 120000/= basi hapa utajua ya kuwa faida yako ni 20000/= sasa unapoenda kujaza fomu ya kuuza vipande kuna sehemu unaweza kuamua kujaza idadi ya vipande unavyouza au ukaamua kujaza eneo ambalo

linasema kiasi cha pesa ambacho unataka kutoa, sasa unaweza kuamua kujaza eneo ambalo linasema kiasi cha pesa na hapa unaweka kiasi ambacho ni faida na unaacha mtaji, na kwa kufanya hivi unakuwa umetoa faida na mtaji umebaki.

Wachaona kiasi cha pesa ambacho unataka kutoa, sasa unaweza kuamua kujaza eneo ambalo linasema kiasi cha pesa na hapa unaweka kiasi ambacho ni faida na unaacha mtaji, na kwa kufanya hivi unakuwa umetoa faida na mtaji umebaki.

SCHEME NAME:

S.No.	Investors Account No.	Name of 1st Unit holder/Beneficiary	No. of Units to be Repurchased (*)	Repurchase Amount in Tshs. (*)

(*) Please furnish the details of either 'Number of Units to be Repurchased' or 'Repurchased amount' (but not both)

Hapo unaona kiboksi cha mwisho kabisa kinakuonyesha ujaze kiasi ambacho unataka kutoa (hii ni fomu ya kuuza vipande)

MIFUKO YENYE HISA NA MIFUKO ISIYO NA HISA

Kama tulivyoona hapo juu kuna kupanda na kushuka kwa mrejesho wa mifuko ambayo imewekeza katika hisa, hivyo kama unakuwa umewekeza katika mifuko hii kuna uwezekano wa mtaji wako kuwa unapungua au kuongezeka, na hii kwa baadhi ya watu inaweza kuwa ni changamoto kwao, ila kuna sifa nyingine ambayo mifuko hii inayo ambayo mifuko isiyo na sera ya kuwekeza katika hisa haina nayo ni uwezekano wa kuwa na mrejesho mkubwa kuliko mifuko isiyo na hisa, mfano tumeona baadhi ya mifuko ina mrejesho wa 51% kwa mwaka kitu ambacho hauwezi kupata katika mifuko isiyo na hisa.

Kwa hiyo unaweza kuangalia uwezekano wa kuwekeza huku pia katika mifuko yenye sera ya kuwekeza katika hisa kama wewe una mpango wa kuwekeza kwa muda mrefu pia unaweza kuwekeza katika mifuko yenye hisa na ambao haina hisa kama mkakati wako wa uwekezaji kwani kwa kufanya hivi utapata faida katika mifuko yenye hisa endapo kutakuwa na faida kubwa kule na pia hautakuwa na mapungufu ya mtaji endapo unakuwa umewekeza katika mifuko isiyo na hisa

JE MFUKO UNATOA GAWIO NI BORA KULIKO USITOA GAWIO?

Jibu ni ndio au hapana kutegemeana na mahitaji ya muwekezaji, kama unahitaji kuwa unapokea pesa mara kwa mara kutoka katika uwekezaji wako basi mfuko unaotoa gawio utakufaa ila kama hauna shida ya gawio basi mfuko ambao hautoi gawio hauna shida yoyote endapo unakuwa umewekeza kule.

Nikupe mfano chukulia una mifuko miwili ambayo imewekeza eneo moja na mrejesho kwa mwaka huo ulikuwa 15% kwa mifuko yote ila mfuko mmoja unatoa gawio na mwingine hautoi gawio unadhani mfuko gani ni bora? Hakuna mfuko bora kuliko mwingine ila inategemea mahitaji ya muwekezaji, kwa yule ambaye anataka pesa yake iendeleo kuzaa tu kwa miaka mingi ijayo mfuko bora kwake ni usiolipa gawio ila kwa mtu ambaye anataka gawio la mara kwa mara basi mfuko unaotoa gawio ndio utamfaa.

Kwa hiyo kama umewekeza UTT AMIS faida yako itakufikia kwa namna hizo mbili.

JINSI YA KUJUA BEI YA KIPANDE

Ukitaka kujua bei ya kipande unaweza kwenda katika tovuti ya UTT AMIS katika kipengele NET ASSET VALUE (thamani ya vipande), au ukatumia APP ya UTT AMIS ambayo utaipata GOOGLE PLAYSTORE kwa jina la UTT AMIS.

UWEKEZAJI WA MARA MOJA NA UWEKEZAJI WA MARA KWA MARA

Kutokana na riba ya kampaundi ya UTT AMIS, basi muwekezaji ambaye anawekeza pesa yake kwa mara moja anakuwa na faida kubwa zaidi kuliko muwekezaji ambaye anawekeza mara kwa mara.

MFANO

Tuchukulie wawekezaji wawili wameanza kuwekeza katika mfuko wa WEKEZA MAISHA, na wote wakachagua ya kuwa katika mpango wao watawekeza 1 milioni, ila muwekezaji wa kwanza akawa anawekeza 8340/= kila mwezi na muwekezaji wa pili akaamua kuwekeza pesa yote kwa pamoja tuone matokeo yao kwa miaka 10. tuchukulie mfuko una mrejesho wa 13 kwa mwaka

Baada ya uwekezaji kuisha muwekezaji wa kwanza aliyekuwa anawekeza kidogo kidogo anakuwa na jumla ya 2057300 (milioni mbili na elfu hamsini na saba na mia tatu) hii ni mtaji pamoja na faida

Muwekezaji wa pili ambaye aliwekeza pesa yote kwa pamoja baada ya uwekezaji kuwa umeisha anakuwa na 3394500 (milioni tatu na laki tisa na elfu nne mia tano)

Kwa hiyo unaweza kuona ya kuwa ijapokuwa kiasi ambacho waliwekeza katika kipindi chote ni 1 milioni, ila yule aliyewekeza pesa yote kwa pamoja amekuwa na faida kubwa kuliko yule aliyewekeza kidogo kidogo kwa sababu pesa yake ilikuwa na muda wa kutosha kufanya kampaundi

Ninachokisema hapa ni kuwa unapowekeza pesa yako kwa mara moja basi inaweza kukuzalia faida kubwa kuliko ukiwekeza kidogo kidogo hata kama mwisho wa siku kiasi ambacho mnakuwa mmewekeza kinakuwa sawa.

Kutokana na uwezo wako kama ukiwa hauna uwezo wa kuwekeza pesa yote kwa pamoja basi hakuna shida ila ukipata nafasi ya kuwekeza pesa yote kwa pamoja basi itumie.

MPANGO WA KUWEKEZEWA GAWIO (RE-INVESTMENT) MPANGO BORA WA UTT AMIS.

Mpaka sasa tumeona mipango mingi ya jinsi ya kuwekeza UTT AMIS, ila ngoja nikupe mpango ambao nadhani ndio bora kuliko yote.

Mpango wa kuwekezewa GAWIO ndio nadhani ni mpango bora kuliko yote kwa wale wanaotaka kuwekeza kwa muda mrefu. Kwa nini nimesema hivi

Kumbuka mwazoni kabisa wakati tunazungumzia faida za kuwekeza UTT AMIS kuwa ni riba ya kampaundi. Sasa mpango huu unatumia riba hii kwa ubora wake ngoja nikupe mfano.

MFANO

Chukulia una vipande 10000 vya mfuko wa HATI FUNGANI na uko katika mpango wa kuwekezewa gawio (re- investment) sasa ina maana gawio likitoka mwezi huu la TSH 1 kwa kipande maana yake ni kuwa utapokea TSH 10000/= na hii pesa itatumika kukununulia vipande tena (tuchukulie umenunuliwa vipande 100) sasa unakuwa na jumla ya vipande 10100, mwezi unaofuata hivi vipande vinapokea tena gawio ambalo sasa litakuwa TSH 10100/= (tuchukulie gawio ni TSH 1 kwa kila kipande), sasa hili gawio linatumika tena kukununulia vipande (tuchukulie umepata vipande 100) jumla unakuwa na vipande 10200, na hivi vipande tena mwezi unakuja vinapokea gawio ambapo kama itakuwa TSH 1 kwa kila kipande basi gawio lako litakuwa TSH 10200/=:, na hii ndio tunaitwa riba ya kampaundi.

Kwa mpango wa kuwekezewa gawio ina maana riba hii inafanya kazi kila mwezi, miezi 3, miezi 6 na sio mara moja kwa mwaka.

Kwa hiyo utaona ya kuwa katika mipango ya kuwekezewa gawio ni kuwa unapokea gawio na gawio pia linapokea gawio.

JINSI YA KUTENGENEZA PENSHENI YAKO.

Moja kati ya ubora wa kuwekeza UTT AMIS ni uwezo wa kutengeneza peshehi yako, sasa hapa ni rahisi mno unachotakiwa kujua ni vitu vitatu

- 1) Kiasi cha pesa ambacho unakihitaji kama peshehi
- 2) Muda ambao utatumia kuwekeza
- 3) Wastani wa mrejesho wa mfuko

MFANO

Chukulia mimi nina miaka 27 na ninataka nikifikisha miaka 57 niwe na peshehi ya milioni 200, je itanilazimu kuwekeza kiasi gani kila mwezi au kwa mara moja ili nifikie lengo lango la kuwa na milioni 200 nikifikisha miaka 57

Hapa ina maana kwa mfuko ambao una mrejesho wa 13 itanibidi kuwekeza $45300/=$ kila mwezi na nitakapofikisha miaka 57 nitakuwa na milioni 200

Kama ninataka kuwekeza kwa mara moja basi kwa mfuko ambao una mrejesho wa 13 basi nitatakiwa kuwekeza milioni 5 tu na baada ya huo muda nitakuwa na milioni 200 kama peshehi yangu

Sasa kwa kuwa mifuko mrejesho wake unabadilika badilika basi unaweza kufikia lengo lako mapema au ukachelewa kutegemea na mrejesho wa mfuko huo ulikuwaje kwa kipindi chote

KWA MAELEZO ZAIDI SOMA KIAMBATANISHO AMBACHO KIKO PAMOJA
NA KITABU HIKI chenye jina jinsi ya kutumia kikokotozi cha UTT AMIS
kutengeneza pensheni yako.

UTT AMIS VS NYUMBA

Unaweza kufanya ulinganisho wa UTT AMIS na uwekezaji mwingine endapo utataka kufanya hivyo. Ila hapa naomba tuangalie mtu anayetaka kuwekeza katika nyumba ya kupangisha na mtu ambaye anawekeza UTT AMIS ni yupi anakuwa na faida nzuri au ambaye uwekezaji wake una tija.

Tutalinganisha nyumba na UTT AMIS katika maeneo yafuatayo

- 1) Mrejesho wa uwekezaji
- 2) Ukwasi
- 3) Hatari za uwekezaji
- 4) Kodi na gharama nyingine.

MREJESHO WA UWEKEZAJI

Nimejenga nyumba na nilikuwa naweka rekodi nzuri tu na wewe kama umejenga au unakusudia kujenga nadhani unaweza kuwa na hesabu zako ambazo unaweza kuzitumia kufanya ulinganisho (hapa nitatumia hesabu za kawaida tu na za kufikirika)

Kiwanja ambacho unaweza kujenga vyumba 12 vya wapangaji kinaweza kukugharimu kati ya milioni 5 mpaka 20 kwa baadhi ya maeneo, tuchukulie hesabu ya milioni 10 na nyumba ya kupangisha vya vyumba 12 ambavyo vinajitegemea vya kisasa, kukiwa na umeme na maji na choo inaweza kukugharimu kati ya milioni 70 mpaka milioni 150 au zaidi kwa baadhi ya maeneo, tuchukulie hesabu ya milioni 100.

Sasa nyumba hii ina wapangaji 12 ambao kila mmoja anatoa 50000/= kila mwezi na jumla ya pesa inakuwa 7.2 milioni, hii ni sawa na asilimia 6.5% ya mrejesho wa uwekezaji kila mwaka (ikiwa mtaji ambao umeingiza ni 110 milioni, kujenga pamoja na kiwanja). Lakini tumeona ya kuwa kama umewekeza UTT AMIS unaweza kuwa na mrejesho wa wastani wa 12 – 15% kwa mwaka

UKWASI WA UWEKEZAJI

Ukwasi maana yake ni ule urahisi wa kubadilisha uwekezaji wako kuwa pesa.

Sasa kama una nyumba utajua ya kuwa sio rahisi kuuza nyumba yako kama unataka kufanya hivyo na inaweza kukuchukua muda mrefu kabla haujapata mteja ila kwa mifuko ya UTT AMIS pesa yako unaipata ndani ya siku 3 au 10 za kazi endapo unakuwa una ihitaji.

1) HATARI ZA UWEKEZAJI

Unapojenga na kupangisha nyumba unakuwa unabeba hatari za uwekezaji kubwa kuliko aliyewekeza UTT AMIS, kuna majanga ya asili ambayo yanaweza kuikumba nyumba, pia wapangaji wako wanaweza kuharibu nyumba na ikakubidi kuwa unafanya ukarabati wa nyumba mara kwa mara.

Kitu kingine ni kuwa wapangaji wanaweza kuwa hawalipi pesa kwa wakati, hizi ni baadhi ya hatari za uwekezaji ambazo unaweza kukumbana nazo endapo unakuwa umewekeza katika nyumba

Hatari ambazo unabeba endapo unakuwa umewekeza UTT AMIS ni ndogo mno.

KODI NA GHARAMA NYINGINE.

Nyumba iwe ya kawaida au ya kibiashara lazima utalipa kodi na hii inapunguza faida ambayo unaipokea.

Pia ukitaka nyumba yako iwe salama lazima uilipie bima kila mwaka, na bima hii inapunguza faida ambayo unaipata kila mwaka

Kwa hiyo unaweza kuona ukiachana na gharama za kufanya marekebisho ya nyumba kuna bima na kodi ambazo zote zinatakiwa kulipwa katika faida ambayo inapatikana kila mwaka na hivyo kupunguza faida.

Sasa wapi panafaa kuwekeza pesa yako, huo ni uchaguzi wako sasa ila kama unataka kuwekeza kwa faida ya juu nadhani UTT AMIS inaweza kuwa sehemu sahihi.

HITIMISHO

Natumaini umejifunza mengi sana katika kitabu hiki na unaweza kuwekeza kwa ujasiri, kama utahitaji kitabu chochote basi usisite kuwasiliana na mwandishi kwa mawasiliano ambayo nimetoa mwanzo na mwisho wa kitabu, pia kama una swali usisite kuuliza muda wowote. Kwa mawasiliano ambayo nimeyatoa

Contact Us

2nd Floor Sukari House,

Sokoine/Ohio Street,

P.O. Box 14825,

Dar es Salaam, TANZANIA

Phone: +255 (0) 22 2128460 / 2122501 /
2137592

Fax: +255 22 2137593.

Email: uwekezaji@uttamis.co.tz

Toll Free Numbers (Namba za bure):

Vodacom, +255 (0) 754 800 544 & 255

(0) 754 800 455. Tigo, +255 (0) 715 800

544 & +255 (0) 715 800 455. Airtel, +255

(0) 782 800 455.



TOVUTI YA UTT AMIS

Website: www.uttamis.co.tz

REFERENCES

- 1) UTT AMIS websites www.uttamis.co.tz
- 2) Umoja fund offer document 2021 edition
- 3) Wekeza maisha offer document
- 4) Watoto fund offer document
- 5) Jikimu fund offer document
- 6) Liquid fund offer document
- 7) Bond fund offer document
- 8) 2021 respective annual reports of all schemes
- 9) Umoja fund trust deed

All of the sources above are available on UTT AMIS website for reference...